

# TURKAN COUNTY GOVERNMENT



## EXECUTIVE OFFICE OF THE GOVERNOR

**SPEECH BY HIS EXCELLENCY HON. JOSPHAT KOLI NANOK, EGH, GOVERNOR - TURKANA COUNTY ON THE OCCASION OF PRESIDING OVER THE 10TH MASHUJAA DAY CELEBRATIONS, OCTOBER 20TH, 2019 AT MOI GARDENS, LODWAR.**



**Deputy Governor, Turkana County,  
Hon. Senator,  
Rt. Hon. Speaker of Turkana County Assembly,  
The Woman Member of Parliament,  
Honorable Members of Parliament,  
Honorable Members of the County Assembly,  
The County Commissioner,  
The County Attorney,  
Officials from the County Government and the National Government,  
Religious Leaders,  
Distinguished Council of Elders,  
Sovereign People of Turkana County.**

**Ladies and Gentlemen**

**My fellow Kenyans,**

We are gathered here once again to mark this important National Day in our calendar to commemorate and appreciate our national heroes and patriots who participated in development of our great nation. From the great sacrifice made by our founding fathers in the fight for our liberation and independence to all the great men and women who have contributed to nation building in post-independence Kenya.

I wish to recognize, all who have continued to work hard to contribute to the realization of the transformative agenda of Turkana County Government. They include all public servants who continue to discharge their duties to the public diligently, the private sector players and the business community that have partnered with us to transform the lives of our people.

### **Water Development, Mineral Exploitation and Natural Resources Management**

My administration is focused to comprehensively address the challenge of access to clean drinking water for both domestic and livestock use. Utilizing our drilling equipment, 18 new boreholes have been drilled and equipped in the past one year across the County, survey for 15 water pans for de-silting purposes have already been done and plans are underway to procure de-silting works, At

Napus junction in Kibish, we have struck a small aquifer with a borehole yielding 35,000 litres per hour, this will eventually be crucial in solving multiple water needs for the residents. Our Operations and Maintenance teams have responded swiftly to reported breakdowns in the water infrastructure and facilities in all the seven Sub counties to allow our people maximum possible access to water.

Last month I launched the Napuu Water Supply Project, contracted to the National Water Harvesting and Storage Authority (NWHSA). Through the project a 300,000 litre-steel tank will be installed at Narewa in Lodwar and a water distribution system set up to benefit 16,000 residents of Narewa, Lokitela, Ekaales, Methewan Kasarani, Juluk and Trans-Africa Secondary School and Turkana University College (TUC). The first phase will cost 72million shillings and will be complete in the next three months.

Through the County Water Department, we have rehabilitated water supplies in Lopeduru together with our development partners at a cost of 12 million shillings. Technical design works for Lokichar and Kangirisae water supply and distribution systems are now complete and the tendering process will start soon, these projects will cost 30 million shillings.

We have further rehabilitated solar systems in Nadapal, Lomeleku, Nakurio and Locher Angikalalio to improve water supply and access, which will benefit over 20,000 persons and 30,000 livestock units.

We intend to equip 76 more boreholes in Turkana Central and Loima Sub-Counties in a programme projected to benefit 80,000 people. So far, we have successfully carried out test pumping of eight boreholes at Sopel, Natir, Koono, Lokiriama, Locher-alomala, Lochor-esekon, Lokuyen and Natwel; equipping of seven boreholes with solar systems in Sopel, Natira, Koono, Kakamera, Lokuyen, Kaekoreakwaan, Lochor-alomala and Natwel.

The new Kakuma Water supply system constructed in the last financial year has brought a big relief to the residents of Kakuma town and its environs. Plans for the implementation of a 500 million shillings Turkana West Water Projects are in top gear as we are finalizing project proposals with implementing partners. The designs and survey for rainwater harvesting structures, rock catchments and rehabilitation of water supplies for Kakuma are complete.

Feasibility studies for medium size dams have been completed for Lokwanamor in Turkana North, Lomelo in Turkana East, Kadokorinyang in Turkana Central and Kalemngorok in Turkana South. The technical designs for these projects are now being developed to inform the procurement stage.

My administration has gazetted the County Environment Committee, whose mandate will be to ensure proper management of environment, including pollution control, waste management and afforestation.

The government has maintained records on the crude oil moving out of the County. A total of 2354 trucks equivalent to 353,100 barrels of crude oil were transported out of the Lokichar Oil Fields by mid-October this year. We shall insist that the revenue from the oil are shared according to the formula already set out in law.

### **Lands, Energy, Housing and Urban Areas Management**

The County government and the people of Turkana must safeguard their land rights and natural resources while promoting development. Land is our identity and resource for the present and future generations. The demand for land has considerably increased in the recent years.

As the Trustees, we will ensure that land access, use, administration and management benefit the local people. The position of government is that anybody requiring community lands for commercial or development should follow the due process of law including community consultations and participation.

### **Ladies and gentlemen,**

The implications of the intended rollout of the Community Lands Act are yet another challenge we should anticipate and deal with. Even when I was the Chairman of Council of Governors, I raised many objections on the practical application of this law on pastoralists' lands. More specifically, the law enacted downplays the critical role of the County government on matters such as registration of land and compensation for community lands after registration.

The department of lands in working together with development partners launched the first GIS Lab (Geographical Information System) in July this year. The County is in the process of procuring modern survey equipment and

software to fully equip the lab and enhance accuracy and precision in mapping. We have initiated spatial planning for Kalobeyei corridor as part of plans to confer municipality status to Kakuma/Kalobeyei.

In compliance with Urban Areas and Cities Act and in the spirit of bringing services closer to the people, I have nominated members of Lodwar Municipality Board and forwarded the names to the County Assembly for vetting and approval before appointment. Meanwhile, an acting municipal manager has been appointed to spearhead affairs of the municipality until the board is fully constituted.

Projects under Kenya Urban Support Program, funded by World Bank, for the Lodwar municipality are ongoing, including installation of solar powered streetlights and floodlights. Works to establish a fire station, which is part of the program, are set to begin soon with the contractor awarded the tender.

To enhance energy access across the County, my administration has entered into public private partnership with three companies engaged in electricity generation, distribution, metering, operation and maintenance.

### **Tourism, Culture and Natural Resources**

Last August, we held the fifth Turkana Tourism and Cultural Festival, Tobong’u Lore 2019. The festival uses celebration of culture to build social cohesion, encourage integration and conflict prevention to foster an enabling environment for investments and sustainable economic development.

Since inception, Tobong’u Lore has received overwhelming support and recognition from communities, development partners and governments of Kenya, Uganda, South-Sudan and Ethiopia. This year, the number of local, regional and international participants increased to over 10,000 with marked corresponding increase in revenue injected into the County economy from expenditures by the participants.

The department of Culture is striving to propose strategies that would make this festival sustainable and affordable to run in the near future.

To enable communities lead efforts to preserve natural resources, my government has registered 16 Community forest associations and certificates are ready to be handed over.

## **Ladies and Gentlemen**

### **Food and Nutrition Security**

In the last one year, 7826 acres of land was put under maize production yielding 109564 bags of 90kg translating to 14 bags per acre, while 12,475 acres was put under sorghum production yielding 199,600 bags of 90kg translating to 16 bags per acre. A total of 309,164 people across the County directly benefited from this cereal harvest. More land was utilized for fruits and vegetable production providing additional food supplements to our people. This yield would have been greater but the effects of the drought experienced in the Country in the past year negatively affected farm outputs.

To further increase crop production, we have surveyed and mapped out all the possible arable lands for irrigation and with the potential for commercial farming along our main rivers of Turkwel, Kerio and Tarach. The Department of Agriculture has established flood-based farming system at Nasinyono, Kalemngorok, Naipa, Loyal, Lokamarinyang and Nadung'a which make up a total of total 1,450 acres; and 40 acres under spate Irrigation at Locheremeyan in Loima Sub County.

The government has carried out disease and vector control countywide. Following this exercise, 1,033,277 shoats were vaccinated against PPR and dewormed benefiting 4,367 households with 102,309 cattle, 6,332 camels, 379,589 shoats and 125 donkeys getting treated against various diseases. As part of support to cushion pastoralists from effects of drought, 2690 bags of livestock feeds were distributed to 5380 pastoralists, and we plan to procure 3148 more bags in the next three months.

Through the fisheries department, we have procured 5 extension motorbikes and trained 90 beach management officials to develop their capacity for proper fisheries resource management. Plans are underway to procure 60 outboard boat engines together with 200 wooden boats for distribution to our fisherfolk to support their livelihoods by increasing fish catches. To avoid post harvest losses, we are procuring 10 solar freezers for Kerio Ward and link the fisherfolk to Lodwar fresh fish market. To expand market access for our fishermen, we have linked Impressa beach management unit in Kalokol with Ceer Fish Processing Company in Nairobi and so far 9 tonnes of fish has been sold.

Friday this week, I launched the Turkana County Livestock Market Days for established markets in Lodwar, Kakuma and Lokichar. The market days will support efforts to commercialize livestock keeping by increasing market access and livestock sales beyond the current rates.

## **Fellow County Residents**

### **Peace Building and Borderlands Initiatives**

Our County shares international borders with Uganda, South Sudan and Ethiopia including internal borders with neighbour counties. With this reality in mind, my administration continues to invest in peaceful, stable and sustainable cross border engagements with our neighbours to create the right environment for development to thrive within the County for the benefit of our people.

These efforts have delivered significant results considerably reducing cases of resource-based conflicts and loss of lives and property to our people in the past 6 years. Relative calm has returned to our borderlands translating to more time spent on productive activities to generate wealth.

Last Month, I was honored to witness the historic signing of the Kenya-Uganda Memorandum of Understanding for Cross-border Peace and Development presided over by Presidents Uhuru Kenyatta and Yoweri Museveni.

The agreement aims at achieving long lasting peace and sustainable development of communities living across the Kenya-Uganda border. This is a huge milestone in our investments in peace building efforts. It will enable governments and partners develop amicable resource-sharing mechanisms, joint infrastructure improvements, youth empowerment as well as supporting cultural activities.

I am happy our president took note of our great need for investment in water infrastructure for livestock production. Already a team of experts has been to Namoni-a-ng'ikaala in Loima sub-county where the Government has committed to construct a dam to benefit pastoralists in the area.

Together with other Turkana leaders, I was part of a Kenyan delegation to Kapoeta State, South Sudan for bilateral meeting on the delimitation and



demarcation of the Kenya–South Sudan boundary as per an agreement between the two countries. Once finalised, both countries will engage in development of the borderlands where conflict over the boundary has contributed to a state of under-development for many years.

### **Fellow Kenyans**

In order to reinstate displaced communities back to their ancestral lands and protect their livelihoods against perennial insecurity, my government commissioned a resettlement programme that began with hard hit Turkana East and Turkana South Sub-counties. These Six projects costing 60 million shillings are at various stages of completion in Turkana East, Turkana South and Loima Sub-Counties

This financial year, we have set aside 140 Million Shillings to undertake fourteen other resettlement sites across the seven sub-counties in order to address problems of vulnerable communities.

### **Public Service, Decentralized Administration and Disaster Management**

The County’s weather outlook indicates that we are anticipating enhanced short rains save for Turkana Central during the October-December window. I call upon all field administrators to sensitize communities and institutions on current weather advisories to avert human suffering and livelihoods losses.

My government will not relent on efforts to cushion the lives of communities affected by drought. The targeted population for this assistance will remain 609,167 persons considered vulnerable. We have already carried out two of the three relief cycles and plans to roll out the final phase of the relief assistance slated for October/ November are at an advanced stage.

My government’s plan to establish the lowest unit of administration is now a reality! In August this year, I signed into law the Turkana County Village Administration Bill 2019. The new legislation will introduce robust government machinery at the village level to deliver services closer to mwananchi at their convenience.

### **Partnerships and Investments**

The development aspirations contained in our County Integrated Development

Plan 2018-2022 require a strategic financing strategy that goes beyond the resources allocated by the national government. My administration will continue to rally and lead integrated development programming and investment efforts from the development partners, the private sector, philanthropies and others to secure the resources needed to actualize the development targets we have set for ourselves.

For example we recently signed an agreement for 500 million shillings five-year programme that aims to address causes of malnutrition through improved access to quality health services and better food and nutrition security with AFRICARE to benefit households in Katilu and Turkwel Wards.

### **Ladies and Gentlemen,**

Last August, the County Government signed an agreement with the World Bank Group's Kenya Competitiveness Enhancement Program (KCEP) to design and implement business regulation reforms that make it simpler, faster, more efficient and convenient for businesses to start, operate and thrive.

### **Trade, Gender and Youth Affairs**

The County Department of Trade has developed a five-year strategic plan for management of Biashara Centre, which is aimed at positioning the centre as one stop shop for business development services for our young people. The next step is to devolve the Biashara Centre model to the sub counties starting with Kakuma town in Turkana West.

In September, we successfully organized the second edition of the Turkana Business Exchange Forum, which attracted 250 Stakeholders and a number of Macro, Small and Medium Enterprises (MSMEs) who got an opportunity to enhance competitiveness and develop business linkages.

My Administration has begun the process to modernize the Lodwar Fresh Produce Market whose works including completion of perimeter wall and additional canopy, is at the tendering stage. This is will enhance security and improve hygiene for a better business environment.

In collaboration with sector partners, 240 agribusiness entities were trained and linked with various market opportunities, an initiative that supported the

creation of market intelligence system.

### **Health Services and Sanitation**

Good health is critical to people's general wellbeing, economic productivity and County's socio-economic progress. Access to health services has improved from the inter-facility distance of 60 kilometres in 2013 to the current distance of 20 kilometres. The target is to achieve the World Health Organization recommended distance of 5 Km in 2 years.

Through the Community Health services Act, 2018, I am happy to report that our 167 community units, in the whole County are now fully operational and have extended crucial health services to the households, beyond the 228 health facilities

### **My Fellow residents,**

After successful operationalization of Lorugum and Katilu operating theatre, Elelea Sub-county hospital theatre is complete and awaiting handing over by the contractor to the user department.

We intend to recruit more health staff to bridge the Human Resource for Health (HRH) gap within the sector considering that the County Public Service Board is now in place.

We now have a new yellow fever vaccine introduced into routine immunization to protect our children against yellow fever. Turkana has been mapped out among high-risk counties for the fever.

While staying true to our promise to reduce the incidence of cervical cancer in Turkana, the department of health is rolling out a vaccine against cervical cancer targeting girls, ten 10-29 years of age. About 20 health facilities have the capacity to offer cancer screening services in Turkana.

### **Ladies and Gentlemen,**

### **Infrastructure, Transport and Public Works**

My government envisions attaining standard infrastructure development through continued upgrade of existing infrastructure and initiating new ones to ease movement of people and goods and facilitate transport and communication.

We have continued to attain great milestones in this regard. This year, we have completed 1808.07 km and another 330 km of roads projects are under procurement stage. Inventory and survey is currently for a further proposed 1170 Km of road Projects and we intend to start implementation as soon as preliminary requirements are finalised. In this year, we are targeting to grade and gravel 2500 Km.

### **Education, Sports and Social Protection**

Earlier this month, Turkana County became the first County to launch a Child Protection Strategy for 2019-2022 in collaboration with development partners. The strategy will guide efforts to protect children from abuse, neglect and exploitation.

It is my expectation the joint effort that went into drafting the strategy will be witnessed in its implementation.

In recognition of our potential in athletics, Turkana County is expected host national cross-country championships early February 2020.

The ECDE school feeding program has improved in terms of Nutrition supplements of fortified porridge, beans and maize to guarantee all-round meals to our Children. In this financial year, we allocated 158 Million shillings to procure food to feed our ECDE children in third term and early January next year.

Our ECDE enrollment currently stands at 106, 356 with a teacher to pupil ratio of 1:180. The recruitment of 300 more ECDE teachers has been finalized and the teachers will soon be posted to institutions across the county.

Turkana County Education and Skill development Support Fund was fully disbursed in Phase two of Bursary allocation of Kshs 165,670,000 and benefited a total of 19,332 needy students in secondary, colleges and universities.

Technical Vocational Education and Training continues to attract many artisans with the enrolment of trainees increasing from 194 in 2016 to 528 in 2019 in the six operational centers across the County. We acknowledge our partners for the full scholarship granted to 10 undergraduate students who joined Technical Universities in the Country.

## **Resource Mobilization and Utilization Finance and Economic Planning**

I am pleased to report that we have achieved 86 percent on the revenue collection of 53.9 million against the target of 62.5 million in the first quarter of this financial year. This is due to the concerted efforts to streamline our Own Source Revenue. In the last financial year (2018/2019) the revenue collected stood at 175 million against the target of 250 million, which represented 70 percent of the set target.

My government through the Finance and Lands departments has conducted an exercise to ascertain the landowners and the plot sizes within Turkana Central Constituency, especially in Lodwar Township and Kanamkemer wards. The exercise shall be rolled out to other areas soon and is expected to be concluded by December this year. It is now a top priority of government to ensure landowners pay all the outstanding land rates to provide government with the much-needed revenue to continue providing services to the general public.

### **Ladies and Gentlemen**

Before I conclude, I want to inform you that new Turkana Public Service Board members and Secretary/Chief Executive Officer have assumed office and taken up their duties. I wish to welcome them to the County Government and express hope that they will serve residents of Turkana diligently.

Finally, I want to take this earliest opportunity to wish our standard eight and form four candidates sitting their national exams this year, both in public and private schools a word of encouragement and success in their exams and subsequent academic endeavors.

**Have a blessed Mashujaa Day!**

**God Bless Kenya**

**God Bless Turkana County,**

**Asanteni Sana**



# SERIKALI YA KAUNTI YA TURKANA



## AFISI YA GAVANA

**HOTUBA YA MHESHIMIWA JOSPHAT KOLI  
NANOK, EGH GAVANA WA KAUNTI YA TURKANA,  
WAKATI WA MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA  
SIKUKUU YA MASHUJA TAREHE 20 OCTOBA 2019  
KATIKA BUSTANI YA MOI GARDENS, LODWAR.**

**Naibu Gavana, Kaunti ya Turkana,  
Mheshimiwa Seneta,  
Mheshimiwa Spika wa Bunge la Kaunti ya Turkana,  
Mwakilishi wa Wanawake Kaunti ya Turkana,  
Waheshimiwa Wabunge la Taifa,  
Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Kaunti,  
Kamishna wa Kaunti,  
Mwanasheria Mkuu wa Kaunti.  
Maafisa wa Serikali ya Kaunti na ile ya Taifa,  
Viongozi wa kidini,  
Wanachama wa Baraza la Wazee,  
Wananchi watukufu wa Kaunti ya Turkana.  
Mabibi na Mabwana,**

**Wakenya wenzangu,**

Tumejumuika hapa kwa mara nyingine kuadhimisha sikukuu hii ya kitaifa huku tukiwaenzi na kuwatambua mashujaa walioshiriki katika ujenzi wa taifa hili letu tukufu. Tunatambua kujitolea kwa wazee waanzilishi wa taifa hili waliopigania uhuru huku pia tukiwaenzi wananchi watajika, wake kwa waume ambao wamechangia ustawi wa nchi hii tangu tulipojinyakulia uhuru.

Nachukua fursa hii kuwatambua wale wote ambao wameendelea kujizatiti kuchangia utekelezaji wa ajenda ya mageuzi katika kaunti ya Turkana. Hii ni pamoja na watumishi wa umma ambao wanatoa huduma kwa wakazi wa kaunti hii kwa uadilifu, wadau wa sekta ya kibinafsi na jamii ya kibiashara ambao wameshirikiana nasi kubadilisha maisha ya watu wetu.

### **Ustawi wa Maji, Uchimbaji Madini na Usimamizi wa Malighafi**

Serikali yangu imejitolea kushughulikia kikamilifu tatizo la uhaba wa maji safi kwa matumizi ya binadamu na mifugo wetu.

Kwa kutumia vifaa vyetu vya kuchima visima tumechimba visima vipya 18 katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Usorovea wa mabwawa 15 kwa ajili ya kutolewa mchanga umefanywa na mipango iko njiani kutafuta mwanakandarasi wa kazi hiyo. Katika makutano ya Napus huko Kibish tumepata mwamba wa maji na kuchimba kisima kinachotoa lita alfu 35 za maji kwa saa moja. Hii ni



hatua muhimu ya kusuluhisha tatizo la uhaba wa maji kwa wakazi wa eneo hilo. Maafisa wetu wa kiufundi wamekuwa wakichukuwa hatua za haraka kukabiliana na kuharibika kwa miundomsingi na katika Kaunti ndogo saba ili kuwaawezesha watu kupata maji kila mara.

Mwezi uliopita, niliongoza uzinduzi wa mradi wa maji wa Napuu, unaotekelezwa na Halmashauri ya Kitaifa ya Ukusanyaji na Uhifadhi wa maji. Kupitia mradi huo, tangi la maji la chuma litawekwa katika eneo la Narewa huko Lodwar na mfumo wa usambazaji maji kuwekwa ili kuwafaidi wakazi elfu 16 wa maeneo ya Narewa, Lokitela, Ekaales, Methewan Kasarani, Juluk na Trans-Africa mbali na kupeleka maji katika chuo cha mafunzo anuwai cha Kisumu na chuo kikuu cha Turkana. Awamu ya kwanza ya mradi huo utakaogharimu shilingi milioni 72 itakamilika katika muda wa miezi mitatu ijayo.

Kushirikishwa kwa halmashauri ya maji ambayo ni asasi ya serikali kuu kwenye mradi huo ni dhahirisho kwamba utekelezaji wa mradi huo utafanyika kwa ustadi na kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa.

Kupitia idara ya maji ya kaunti, tumekarabati mradi wa maji wa Lopeduru kwa ushirikiano na shirika la utoaji misaada la Kanisa Katoliki kwa gharama ya shilingi milioni 12. Katika maeneo ya Lokichar na Kangirisae, miradi ya maji ilikamilishwa kwa ushirikiano wa hazina ya kitaifa ya sekta ya maji ambayo ilitoa ufadhili wa shilingi milioni 30. Ningependa kupongeza ushirikiano na ufadhili wa washirika hawa katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Aidha tumekarabati miradi ya kawi ya miale ya jua katika maeneo ya Nadapal, Lomeleku, Nakurio na Locher Angikalalio ili kuimarisha utoaji maji na kurahisisha upataji wa rasilimali hiyo. Miradi hiyo itawafaidi wakazi 20,000 na mifugo 30,000.

Tunania kujenga visima vingine 76 katika kaunti ndogo za Turkana ya Kati na Loima chini ya mpango uliokadiriwa kuwanufaisha watu elfu 80. Kufikia sasa tumefanikiwa kufanyia majaribio visima vinane katika maeneo ya Sopol, Natir, Koono, Lokiriama, Locher-alomala, Lochor-esekon, Lokuyen na Natwel Mfumo mpya wa usambazaji maji Kakuma uliojengwa mwaka uliopita umeleta afueni kubwa kwa wakazi wa Kakuma. Mipango ya utekelezaji wa miradi ya maji ya Turkana Magharibi ya gharama ya shilingi milioni 500 inaendelea huku tukikamilisha mapendekezo ya miradi na washirika wetu.

Uchoraji wa mifumo ya ukusanyaji maji ya mvua, miamba ya maji na ukarabati

wa mifumo ya maji eneo la Kakuma umekamilika.

Utafiti wa mabwawa ya kiwango cha kadri umekamilika katika eneo la Lokwanamor Turkana Kaskazini, Lomelo Turkana Mashariki, Kadokorinyang Turkana ya Kati na Kalemngorok Turkana Kusini. Michoro ya miradi hii inaundwa ili kuingia awamu ya kutafutiwa wanakandarasi.

Serikali yangu imeweka kamati ya mazingira ambayo jukumu lake litakuwa kuhakikisha usimamizi bora wa mazingira pamoja na kudhibiti uchafuzi , usimamizi wa taka na kuongeza maeneo ya misitu.

Serikali ya Kaunti imeweza kuweka rekodi ya mafuta yanayotolewa kutoka kaunti yetu. Jumla ya malori 2,354 ambayo ni sawa na mapipa 353,100 yalisafirishwa nje ya visima vya Lokichar kufikia katikati ya mwezi huu wa Octoba.

Tutasisitiza kwamba mapato ya mafuta tupate fungu letu kuambatana na sheria iliyowekwa

### **Ardhi, kawi, nyumba na usimamizi wa miji**

Serikali ya kaunti na watu wa Turkana lazima walinde haki zao za ardhi na mali asili huku wakiimarisha ustawi wa kiuchumi. Ardhi ni kitambulisho chetu na mali asili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Hitaji la ardhi limekuwa likiongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni.

Kama wadhamnini, tutahakikisdha ya kwamba upatikanaji, matumizi, na usimamizi wa ardhi unawafaidi wakazi wa kaunti hii. Msimamo wa serikali ni kwamba mtu yeyote anayehitaji kutumia ardhi ya kijamii kwa shughuli za kiuchumi au ustawishaji ni lazima afuate utaratibu uliowekwa ikiwemo kushauriana na kushirikisha jamii.

### **Mabibi na mabwana,**

Athari za uzinduzi wa sheria ya ardhi ya kijamii iliyopendekezwa bado ni changamoto nyingine ambayo lazima tukadirie na kukabiliana nazo. Hata wakati nilipokuwa mwenyekiti wa baraza la magavana niliibua wasiwasi kuhusu utekelezaji kikamilifu wa sheria hiyo katika ardhi ya wafugaji. Sheria hiyo hata hivyo inadunisha wajibu muhimu wa serikali ya kaunti kwenye masuala ya usajili wa ardhi na kulipwa fidia kwa ardhi ya kijamii baada ya usajili.

Idara ya ardhi ikishirikiana na washirika wa maendeleo ilizindua maabara ya

kwanza ya mifumo ya habari kuhusu ardhi, mwezi Julai mwaka huu. Serikali ya kaunti iko katika harakati za kununua mfumo wa kisasa wa usoroveya pamoja na software ili kuwezesha maabara hayo kutoa habari sahihi na ya kuaminika kuhusu ardhi.

Tumeanzisha mkakati wa mpango wa eneo la Kalobeyei kama sehemu ya mipango ya kupandisha hadhi eneo la Kakuma/Kalobeyei na kulifanya manisipaa.

Kwa kuzingatia sheria ya maeneo ya miji na kwa nia ya kuleta maendeleo karibu na wananchi, nimependekeza majina ya wanachama wa bodi ya manisipaa ya Lodwar na kuwasilisha orodha hiyo kwa bunge la kaunti ili yaidhinishwe kabla ya uteuzi wao. Wakati huo huo, kaimu Meneja wa Manisipaa hiyo ameteuliwa kuongoza shughuli za mji huo hadi bodi kamili itakapobuniwa.

Miradi iliyoko chini ya Mpango wa Uungaji mkono Maeneo ya Mijini na ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa miinjili ya manisipaa ya Lodwar inaendelea. Hii ni pamoja na kuweka taa za barabarani zitakazotumia kawi ya miale ya jua. Ujenzi wa kituo cha wazima moto ambacho ni sehemu ya mradi huo umepangiwa kuanza hivi karibuni huku mwanakandarasi akiwa tayari amepewa zabuni hiyo.

Ili kuimarisha upataji kawi kwa wakazi wa kaunti, serikali yangu imetia sahihi mkataba na washirika wa kibinafsi ambazo ni kampuni tatu zinazohusika na uzalishaji kawi, usambazaji, uwekaji mita na usimamizi.

### **Utalii, utamaduni na mali asili**

Mnamo mwezi Agosti, tuliandaa makala ya tano ya tamasha za Turkana za utalii na utamaduni al-maarufu Tobong'u Lore 2019. Tamasha hizo hutumika kudumisha utangamano wa kijamii, kuhimiza uwiano na kuzuia mafarakano ili kubuni mazingira mwafaka kwa wawekezaji na kudumisha maendeleo endelevu.

Tangu kubuniwa kwake, tamasha za Tobong'u Lore zimepokea uungwaji mkono mkubwa na kutambuliwa na jamii mbalimbali, washirika wa maendeleo na serikali za Kenya, Uganda, Sudan Kusini na Ethiopia. Mwaka huu, idadi ya washiriki kutoka nyumbani, kanda hii na ulimwengu kwa jumla iliongezeka hadi zaidi ya watu elfu 10. Hatua hii ilifanikisha ongezeko la mapato kwa kaunti yetu kutokana na pesa zilizotumiwa na washiriki wa tamasha hizo. Idara ya utamaduni inajizatiti kupendekeza mikakati ambayo itatuwezesha

kudumisha tamasha hizo kwa gharama nafuu katika siku za usoni.

Ili kuziwezesha jamii kuwa katika mstari wa mbele wa kuhifadhi mali asili, serikali yangu imesajili vyama 16 vya kijamii vya kuhifadhi misitu na vitakabidhiwa vyeti hivyo karibuni.

## **Mabibi na Mabwana**

### **Kujitosheleza kwa lishe na chakula**

Serikali yangu kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo itaendelea na mipango ya pamoja ya kujikimu kwa chakula miongoni mwa jamii. Hii ni pamoja na kuongeza ardhi ambamo mnakuzwa chakula kupitia kukumbatia mifumo ya kilimo inayozingatia mabadiliko ya hali ya anga, matumizi ya mashine katika kilimo, upanuzi wa kilimo cha unyunyiziaji maji mashamba na matumizi mwafaka ya ardhi kwa shughuli za kilimo.

Ili kuongeza ustawi wa kilimo, tumejizatiti kutambulisha na kutoa ramani ya arhi inayoweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji tukiwa na matumaini ya kuanzisha kilimo biashara katika meneo hayo.

Idara ya kilimo imeanzisha kilimo kinachotegemea mafuriko katika maeneo ya Nasinyono, Kalemngorok, Naipa, Loyal, Lokamarinyang na Nadung'a ambayo ni ardhi ya ekari 1,450. Ekari nyingine 40 zitatumika kwa shughuli za kilimo cha kunyunyizia maji mashamba katika eneo la Locheremeyan katika kaunti ndogo ya Loima.

Kuhusu udhibiti wa magonjwa yanayoathri mifugo, serikali ya kaunti ikishirikiana na washirika wa kimaendeleo kama vile UN-FAO, RPLRP, TUPADO, LWF, AFYA TIMIZA na Anglican Development Services (ADS) imeweza kutekeleza shughuli ya utoaji huduma za afya kwa mifugo katika kaunti hii. Kupitia shughuli hiyo, mbuzi na kondoo 1,033,277 zilipata chanjo dhidi ya ugonjwa wa PPR na kupewa dawa za minyoo ambapo familia 4,367 zilifaidika. Aidha ng'ombe; 102,309, ngamia 6,332, mbuzi na kondoo 379,589 pamoja na punda 125 zilipata matibabu dhidi ya magonjwa mbalimbali. Matokeo ya shughuli hiyo ni kwamba tumeweza kudhibiti magonjwa ya mifugo na kuepusha hasara miongoni mwa wafugaji.

Na katika juhudi za kuwakinga wafugaji dhidi ya athari za hali ya kiangazi, magunia 2690 ya chakula cha mifugo yalitolewa kwa Zaidi ya wafugaji wafugaji elfu 5 na tunapania kununua magunia elfu 3zaidi ya chakula hicho

katika muda wa miezi mitatu ijayo.

Mnamo siku ya Alhamisi juma lililopita, nilizindua siku za masoko ya mifugo katika kaunti katika masoko yanayotambulika huko Lodwar, Kakuma na Lokichar, kama sehemu ya ushirikiano wetu na shirika la misaada la Marekani, USAID chini ya mpango wa usimamizi wa mifumo ya soko la mifugo, (LMS). Siku za masoko hayo zitapiga jeki juhudi za kuimarisha biashara ya mifugo na kuwapatia wafugaji fursa ya kujiongezea mapato zaidi ya ilivyo sasa.

### **Miradi ya kudumisha amani na shughuli za mipakani**

Mwezi uliopita, nilipata fursa ya kushuhudia kutiwa sahihi kwa mkataba wa maelewano wa kihistoria wa kuleta amani na ustawi kwenye mpaka kati ya Kenya na Uganda kati ya rais Uhuru Kenyatta na mwenzake Yoweri Museveni.

Mkataba huo unalenga kuleta amani ya kudumu na maendeleo endelevu miongoni mwa jamii zinazoishi kwenye mpaka wa Kenya na Uganda. Hii ni hatua muhimu sana ya juhudi za kuleta amani katika kanda hii. Hatua hiyo itaziwezesha serikali na washirika wake kubuni mikakati ya pamoja ya ugavi wa mapato, uimarishaji wa muundo mbinu, kuwapa vijana uwezo na kupiga jeki shughuli za kitamaduni.

Nina furaha kwamba Rais wetu alitilia maanani haja yetu kubwa ya kuwekeza katika miundo mbinu ya maji kwa minajili ya uzalishaji katika sekta ya mifugo. Tayari, kundi la wataalamu limepelekwa katika eneo la Namoni-a-ng'ikaala katika kaunti ndogo ya Loima ambapo serikali imejitolea kujenga bwawa ili kuwafaidi wafugaji katika eneo hilo. Ni muhimu kutambua kwamba serikali ya kaunti ya Pokot Magharibi imetambulisha eneo ambapo itajenga bwawa katika kaunti hiyo ambapo wafugaji kutoka kaunti ya Turkana na Pokot hulisha mifugo wao.

Pamoja na viongozi wengine wa kaunti ya Turkana, nilikuwa miongoni mwa ujumbe wa Kenya uliotembelea jimbo la Kapoeta, nchini Sudan Kusini kwa mazungumzo ya pamoja kuhusu uratibishaji na uchoraji wa mpaka kati ya Kenya na taifa hilo kuambatana na makubaliano kati ya serikali hizo mbili. Pindi utakapokamilika, mataifa yote mawili yataweza kushirikiana katika ustawishaji wa maeneo ya mpakani ambapo mizozo kuhusu mpaka imezorotesha maendeleo kwa miongo mingi.

## **Wakenya wenzangu,**

Ili kurejesha jamii zilizohamishwa kutoka makazi yao ya asili na kuzilinda jamii dhidi ya athari za kudorora kwa usalama, serikali yangu imebuni mpango wa kuwapa wakazi makao utakaoanza katika kaunti ndogo za Turkana Mashariki na Turkana Kusini ambazo zimeathiriwa zaidi. Miradi sita iliyogharimu shilingi milioni 60 tayari imetekelezwa na kuwafaidi wakazi elfu 15 katika vijiji vya Lomaro, Kakiteitei, Kasarani katika wadi ya Kapedo/Napeitom; Nakot katika wadi ya Lobokat; Lorokon katika wadi ya Kaputir, na Locher-Elim katika wadi ya Lobei/Kotaruk.

Katika kipindi hiki cha matumizi ya pesa za serikali, tumetenga shilingi milioni 140 kuweka maeneo zaidi ya makazi katika kaunti ndogo saba ili kutatua tatizo la ukosefu wa makazi miongoni mwa jamii husika.

## **Utumishi wa umma, utawala uliogatuliwa na usimamizi wa majanga**

Kwa mujibu wa utabiri wa hali ya anga, tunatarajia kupata mvua ya kuridhisha wakati wa msimu huu wa mvua ya vuli isipokuwa katika eneo la Turkana ya kati. Ninatoa wito kwa maafisa wa utawala wote wa nyanjani kutoa hamasisho kwa jamii na taasisi huzika kuhusu hali ya anga iliyoko ili kuepusha masaibu na uharibifu wa maisha.

Serikali yangu haitalegeza kamba katika juhudi za kuikinga jamii dhidi ya athari za ukame. Idadi ya watu tunaolenga kusaaidia kukabiliana na athari hizo ni Zaidi ya watu elfu 600 wanaokadiriwa kuwa katika hatari zaidi. Tayari tumetoa msaada kwao mara mbili kati ya mara tatu na tunapanga kuanzisha awamu ya mwisho ya msaada huo kati ya mwezi Oktoba na Novemba.

Ndoto ya serikali yangu ya kuzindua kitengo cha chini zaidi cha utawala sasa imetimia! Mnamo mwezi Agosti mwaka huu, nilitia sahihi kuwa sheria mswada wa kaunti ya Turkana wa utawala wa vijiji wa mwaka 2019. Sheria hiyo mpya itawezesha uwakilishi wa serikali nyanjani ili kuimarisha utoaji huduma kwa mwananchi kwa njia rahisi.

## **Ushirikiano na uwekezaji**

Maono ya maendeleo yaliyomo kwenye mkakati wa pamoja wa maendeleo

wa mwaka 2018-2022 yanahitaji mpango mahsusi wa kifedha unaopiku pesa tunazotengewa na serikali ya taifa. Serikali yangu itaendelea kuhimiza juhudi za mipango na uwekezaji kwa ushirikiano na washirika wa kimaendeleo, sekta ya binafsi, wahisani na wengineo ili kupata pesa zinazohitajika kutimiza malengo yetu ya mendeleo.

Kwa mfano hivi majuzi tulitia sahihi mkataba wa mpango wa miaka mitano utakaogharimu shilingi milioni 500 ambao unalenga kushughulikia maradhi ya utapiamlo kupitia kwa utoaji huduma mwafaka za afya utoshelevu wa chakula na lishe kati ya serikali yangu na shirika la AFRICARE ili kuwafaidi wakazi wa wadi za Katilu na Turkwel.

### **Mabibi na mabwana,**

Mnamo mwezi Agosti, serikali ya kaunti ilitia sahihi mkataba wa makubaliano na shirika la Benki ya Dunia, Kenya Competitiveness Enhancement Program (KCEP) wa kubuni na kutekeleza mabadiliko ya kanuni za kibiashara ili kurahisisha na kulainisha juhudi za kuanzisha biashara, kuzidumisha na kuziwezesha kuimarika.

### **Biashara, jinsia na masuala ya vijana**

Idara ya biashara kwenye kaunti yetu imebuni mkakati wa miaka mitano wa usimamizi wa kituo cha kibiashara kwa jina Biashara Centre. Kituo hicho kinatarajiwa kuwa kitovu cha ustawishaji wa ujasiriamali miongoni mwa vijana wa kaunti yetu. Hatua ifuatayo ni kukigatua kituo hicho katika kaunti ndogo tukianzia na mji wa Kakuma katika eneo la Turkana Magharibi.

Mnamo mwezi Septemba, tulifanikiwa kuandaa makala ya pili ya mkutano wa kibiashara wa kaunti ya Turkana uliowavutia wadau 250 na wenye biashara kubwa, ndogo na za kadri ambao walipata fursa ya kuimarisha ushindani wa kibiashara na kubuni mitandao ya kibiashara kati yao na wenzao.

Serikali yangu imeanzisha utaratibu wa kulifanya soko la Lodwar kuwa la kisasa. Tayari utaratibu wa kutoa zabuni ya ujenzi wa ua kuzunguka soko hilo umeanza. Hii itaimarisha usalama na kuboresha usafi kwa mazingira bora ya kibiashara.

Kwa ushirikiano na wadau wa sekta mbalimbali, kampuni 240 za kilimo biashara zimepata mafunzo na kuuunganishwa na fursa ya kupata masoko, mradi ambao

ulifanikisha kubuniwa kwa mfumo wa habari za masoko.  
Huduma za Afya na Usafi

Afya bora ni muhimu kwa maisha ya wananchi, ustawi wa kiuchumi na kijamii. Upataji huduma za afya umeimarika kutoka umbali wa kilomita 60 kutoka kituo kimoja cha afya hadi kingine tulioshuhudia mwaka 2013 hadi umbali wa kilomita 20 wakatu huu. Maono yetu ni kuafikia lengo la shirika la afya ulimwenguni la kilomita 5 katika muda wa miaka miwili.

Kupitia sheria ya huduma za afya ya umma ya mwaka 2018, nina furaha kuwatangazia kwamba vituo vyetu 167 vya kijamii kote katika kaunti sasa vinatumika na vinatoa huduma muhimu za afya kwa wakazi mbali na vituo vingine 228 vya afya.

### **Wakazi wenzangu,**

Baada ya kufanikisha ufunguzi wa vyumba vya upasuaji katika hospitali za Lorugum na Katilu. Chumba cha upasuaji katika hospitali ya kaunti ndogo ya Elelea kimekamilika na kinasubiri kukabidhiwa kwa idara husika na mwanakandarasi aliyetekeleza ujenzi huo.

Tunatarajia kuwaajiri wafanyikazi zaidi wa afya ili kuziba nakisi iliyoko kwenye sekta hiyo huku ikizingatiwa kwamba bodi ya huduma za umma ya kaunti imeanza kutekeleza majukumu yake.

Tumeanza kutoa chanjo dhidi ya homa ya manjano (yellow fever) kama sehemu ya kuwakinga watoto wetu dhidi ya ugonjwa huo. Kaunti ya Turkana imeorodheshwa miongoni mwa kaunti zilizo katika hatari ya mfumko wa ugonjwa huo.

Na katika juhudi za kutimiza ahadi yetu ya kupunguza idadi ya visa vya saratani ya mlango wa kizazi katika Kaunti ya Turkana, idara ya afya imeanzisha chanjo dhidi ya ugonjwa huo inayowalenga wasichana wa kati ya miaka 10 na 29. Takriban vituo 20 vya afya katika kaunti ya Turkana vina uwezo wa kuchunguza maradhi ya saratani.

### **Mabibi na Mabwana**

#### **Muundo msingi, uchukuzi na ujenzi**

Serikali yangu inadhamiria kutimiza viwango vinavyotakikana katika ustawi



wa muundo msingi kupitia ukarabati wa miundo msingi iliyoko na kuanzisha miradi mipya ili kurahisisha shughuli za uchukuzi kwa wakazi na bidhaa mbali na kuimarisha mawasiliano. Tumeendelea kupiga hatua kubwa katika jitihada hizi. Mwaka huu, tumekamilisha miradi ya kukarabati kilomita elfu 18 za barabara na tumeanzisha utaratibu wa kutoa zabuni za miradi ya ujenzi wa kilomita nyingine 330. Shughuli za usoroveya wa miradi ya barabara za kilomita 1170 zilizopendekezwa zinaendelea na tunapania kuanzisha utekelezaji wa miradi hiyo pindi masharti yaliyoko yatakapotimizwa. Mwaka huu, tunatarajia kukarabati barabara za kilomita 2500.

### **Elimu, michezo na maslahi ya kijamii**

Mapema mwezi huu, kaunti ya Turkana ilikuwa ya kwanza kuzindua mkakati wa ulinzi wa watoto wa mwaka 2019-2022 kwa ushirikiano na washirika wa kimaendeleo. Mkakati huu utatoa mwongozo katika juhudi za kuwakinga watoto dhidi ya dhuluma, kutelekezwa na kunyanyaswa.

Ni matarajio yangu kwamba juhudi hizi za pamoja zilizoshuhudiwa wakati wa kubuni mkakati huo zitadhihirika wakati wa utekelezaji wake.

Katika kutambua umahiri wetu katika nyanja ya riadha, kaunti ya Turkana inatarajiwa kuandaa mashindanio ya kitaifa ya mbio za nyikani mwezi Februari mwaka 2020.

Mpango wa utoaji chakula katika shule za chekechea umeimarika kupitia utoaji wa virutubishi na uji, maharagwe na mahindi yaliyoimarishwa ili kuhakikisha watoto wetu wanapata lishe ya kutosha. Katika kipindi hiki cha matumizi ya pesa za serikali, tumetenga shilingi milioni 158 kununua chakula kuwalisha watoto wetu wa shule za chekechea katika muhula wa tatu na mapema mwakani.

Kwa sasa, idadi ya watoto wanaojiunga na shule za chekechea katika kaunti yetu ni 106, 356 huku kila mwalimu akisimamia takriban watoto 180. Uajiri wa walimu 300 zaidi wa chekechea umekamilika na watapelekwa katika shule mbalimbali katika kaunti.

Hazina ya ustawi wa elimu na ujuzi katika kaunti ya Turkana ilitolewa kikamilifu katika awamu ya pili ya utoaji ufadhili wa masomo wa jumla ya shilingi milioni 165 elfu 670 ambao uliwafaidi Zaidi ya wanafunzi elfu 19 kutoka familia maskini walioko katika shule za upili, vyuo anuwai na vyuo vikuu.

Mafunzo ya kiufundi yanaendelea kuwavutia wasomi wengi huku idadi ya

wanafunzi walioujiunga na vyuo vya mafunzo ya kiufundi ikiongezeka kutoka 194 mwaka 2016 hadi 528 mwaka huu 2019 katika taasisi sita zilizoko katika kaunti hii. Tunatambua washirika wetu kwa kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 10 walioujiunga na vyuo vikuu vya kiufundi kote nchini.

### **Ukusanyaji na utumizi wa mapato**

#### **Mipango ya kifedha na kiuchumi**

Nina furaha kutangaza kwamba tumefikia lengo la asilimia 86 la ukusanyaji ushuru ambao ni jumla ya shilingi milioni 53 nukta 9 dhidi ya lengo letu la shilingi milioni 62 nukta 5 katika robo ya kwanza ya kipindi hiki cha matumizi ya pesa. Hii imetokana na juhudi za pamoja za kulainisha mfumo wa ukusanyaji mapato yetu sisi wenyewe. Katika kipindi kilichotangulia cha matumizi ya pesa za serikali, (2018/2019) tulikusanya jumla ya shilingi milioni 175 dhidi ya shabaha yetu ya shilingi milioni 250 ambayo ni asilimia 70 ya lengo letu.

Serikali yangu kupitia idara za fedha na ardhi imekamilisha shughuli ya kubainisha wamiliki ardhi na kiwango cha ardhi wanayomiliki katika eneo bunge la Turkana ya kati hususan katika mji wa Lodwar na wadi ya Kanamkemer. Shughuli hiyo itasambazwa katika maeneo mengine hivi karibuni na inatarajiwa kukamilika ifikapo mwisho wa mwezi Disemba mwaka huu. Serikali imezipatia kipaumbele juhudi za kuhakikisha kila mwenye ardhi analipa ada zinazohitajika ili kukusanya mapato yanayohitajika kuiwezesha serikali ya kaunti kutoa huduma bora kwa wananchi.

#### **Mabibi ba mabwana**

Kabla sijatamatisha hotuba yangu, nataka kuwafahamisha kwamba bodi mpya ya utumishi wa umma ya kaunti ya Turkana pamoja na Katibu na Afisa mkuu mtendaji wameanza kutekeleza majukumu yao. Ningetaka kuwakaribisha katika serikali ya kaunti ya Turkana na kuwapa matumaini kwamba watawahudumia wakazi wa kaunti yetu kwa uadilifu.

Hatimaye ningependa kuchukua fursa hii kuwatakia kila la heri wanafunzi watakaofanya mitihani yao ya darasa la nane na kidato cha nne katika shule za umma na za kibinafsi wakati wa mitihani hiyo. Nawatakia ukakamavu na mafanikio katika mitihani yao na katika mipango yao ya kielimu siku za usoni.

**Muwe na sikukuu ya Mashujaa yenye Baraka!**

**Mungu aibariki Kenya**

**Mungu aibariki kaunti ya Turkana,**

**Asanteni Sana**

**Ee Mungu nguvu yetu  
Ilete baraka kwetu  
Haki iwe ngao na mlinzi  
Natukae na undugu  
Amani na uhuru  
Raha tupate na ustawi.**

**Amkeni ndugu zetu  
Tufanye sote bidii  
Nasi tujitoe kwa nguvu  
Nchi yetu ya Kenya  
Tunayoipenda  
Tuwe tayari kuilinda**

**Natujenge taifa letu  
Ee, ndio wajibu wetu  
Kenya istahili heshima  
Tuungane mikono  
Pamoja kazini  
Kila siku tuwe na shukrani**

**Ee Mungu twaomba ulinde  
Jumuiya Afrika Mashariki  
Tuwereshe kuishi kwa amani  
Tutimize na malengo yetu.**

**Jumuiya Yetu sole tuilende  
Tuwajibike tuimarike  
Umoja wetuni nguzo yetu  
Idumu Jumuiya yetu.**

**Uzalendo pia mshikamano  
Viwe msingi wa Umoja wetu  
Natulinde Uhuru na Amani  
Mila zetu Na desturi zetu.**

**Viwandani na hata mashambani  
Tufanye kazi sote kwa makini  
Tujitoe kwa hali na mali  
Tuijenge Jumuiya bora.**